

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA SINGIDA



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na. HM/SI/T.40/13/VOL.XI/102

19 Julai 2021

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida anakaribisha maombi ya kazi kwa Watanzania wote wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi ya **MTENDAJI WA MTA A DARAJA LA III**. Tangazo hili ni kutokana na Kibali cha ajira Mbadala chenye Kumb. Na. FA.170/366/01"B"/18 cha tarehe 14 Juni, 2021 kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora

1.0 MTENDAJI WA MTA A DARAJA LA III - NAFASI 03

1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Awe na cheti cha ufaulu wa Kidato cha Nne (IV) AU Sita (VI) na waliohitimu mafunzo ya Cheti (Astashahada) katika fani zifuatazo: Utawala, Uongozi na Usimamizi wa Fedha, Sheria, Elimu ya Jamii, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo au Chuo/Taasisi yoyote inayotambuliwa na Serikali.

1.2 KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA MTA A DARAJA LA III

- i. Katibu wa Kamati ya Mtaa
- ii. Mtendaji Mkuu wa Mtaa
- iii. Mratibu wa utekezaji wa Sera na Sheria zinazotekelezwa na Halmashauri katika Mtaa
- iv. Mshauri wa Kamati ya Mtaa kuhusu mipango ya Maendeleo katika Mtaa
- v. Msimamizi wa utekezaji wa Sheria ndogo pamoja na Sheria nyingine zinazotumika katika Mtaa.
- vi. Mshauri wa Kamati ya Mtaa kuhusu masuala ya ulinzi na usalama
- vii. Msimamizi wa utekezaji wa mikakati mbalimbali inayohusu uondoaji wa njaa na umaskini katika Mtaa

- viii. Kusimamia ukusanyaji wa Mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu za Walipa Kodi wote
- ix. Kuandaa na Kutunza Rejesta ya Wakazi wote wa Mtaa
- x. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

1.3 MSHAHARA

Kwa kuzingatia viwango vya Serikali yaani ngazi ya Mshahara ya TGS B

1.4 MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45 na usiopungua umri wa miaka 18
- ii. Waombaji wote waambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa na Nakala ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA)
- iii. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina yawadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
- iv. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, nakala za vyeti vya Kidato cha Nne na Kidato cha Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
- v. Picha ndogo moja "Passport size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.
- vi. Testimonials", "Provisional Results", "Statement of results", Hati Matokeoza Kidato cha Nne na Sita, yaani FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS HAVITAKUBALIWA.
- vii. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 3 Agosti, 2021 saa 9:30Alasiri.
- viii. Maombi yanaweza kuandikwa kwa Lugha ya Kiswahili fasaha au Kiingereza fasaha na yatumwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida au kupitia Posta kwa anuani ifuatayo:

MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA SINGIDA,
S.L.P 236, SINGIDA

Imetolewa na:


Bravo K. Lyapembile
Mkurugenzi wa Manispaa
Singida **MKURUGENZI WA MANISPAA
SINGIDA**

Halmashauri ya Manispaa: Karume Road: S.L.P 236, Singida; Simu Na: +255 26 250 2179/2362;
Nukushi Na: +255 26 250 2179; Barua pepe: md.singidamc@singida.go.tz; Tovuti: www.singidamc.go.tz